**Nukuu za familia**



*"Kulea na kuelimisha watoto kwa njia iliyo sahihi ni jukumu kubwa sana na la msingi kwa wazazi, na ustawi pamoja na maendeleo ya taifa hutegemea sana jambo hilo. Ndiyo maana kila mtu anapaswa kulichukulia kwa uzito mkubwa..."* **John Locke**



*"Njia ya busara zaidi ni kumkuza mtoto ili awe mtu mzima, si kumlazimisha mtu mzima awe kama mtoto. Utoto una namna zake za kuona, kufikiri, na kuhisi; hakuna jambo la kipumbavu kuliko kujaribu kubadilisha hivyo..."* **Jean-Jacques Rousseau**



*wake. Ms... kwa katik... to wake ...*

# Latra ichukue hatua thabiti kusimamia tiketi za kielektroniki

Gazeti hili jana lilikuwa na habari iliyosomeka kwamba "Tiketi za kielektroniki bado mfupa mgumu", ikionyesha jinsi utekelezaji wake bado unakabiliwa na changamoto nyingi.

Mapinduzi haya ya teknolojia katika sekta ya usafirishaji nchini Tanzania yalilenga kuleta ufanisi, usalama na uwazi.

Hata hivyo, hali inayojitokeza sasa katika usafiri wa mabasi ya masafa marefu, kama ilivyobainishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (Latra) hivi karibuni, ni kengele ya hatari inayohitaji hatua za haraka na madhubuti.

Ni wazi kuwa mianya ya kurudi kwenye mfumo wa kizamani wa "tiketi za karatasi" bado ipo, na inatumiwa vibaya na walanguzi kuumiza wananchi.

Ripoti ya Latra ya Desemba 2025 inaonyesha taswira ya kusikitisha: Kati ya Sh79 bilioni zilizotokana na miamala ya tiketi mwezi Desemba, ni asilimia 11 tu (Sh4 bilioni) zilizopita kwenye mfumo wa mtandao.

Hii ina maana kuwa asilimia 89 ya fedha bado zinazunguka mkononi, hali inayotoa mwanya wa wazi wa upotevu wa mapato ya Serikali, ubadhirifu kwa wamiliki wa mabasi, na muhimu zaidi, ulanguzi wa bei unaowaumiza abiria.

Ukubwa wa tatizo hili unaashiria jambo moja, kwamba Serikali, kupitia Latra, haina budi kuimarisha usimamizi wa mifumo ya kielektroniki.

Haiingii akilini kuona tiketi moja ikiwa na majina matatu tofauti, moja la mfumo na mengine ya kuandikwa kwa mkono. Huu ni uhujumu wa wazi na lazima jambo lifanyike ili kudhibiti hali hii.

Tunakubaliana na wa wanaoshauri kuunganisha mfumo tiketi na Nida, kama walivyoshauri wamiliki wa mabasi kupitia chama cha Taboa, kuwa mfumo wa tiketi uunganishwe na namba za utambulisho wa Taifa ili kuzuia watu hewa kukata tiketi kwa wingi na kuziuza kwa bei ya juu.

Hatua nyingine muhimu na ya lazima ni kufanya operesheni maalumu endelevu ya kuondoa watu wasio rasmi katika vituo vya mabasi, wapigadebe, ambao wanageuza mfumo wa kielektroniki kuwa chombo cha ulanguzi wa fedha taslimu.

Ukiachana na upotevu wa mapato na ulanguzi wa wa tiketi, kutofautiana kwa taarifa za abiria kati ya manifesto ya basi na uhalisia ni hatari kwa usalama wa Taifa. Endapo ajali itatokea, inakuwa vigumu kutambua wahusika au kutoa taarifa kwa ndugu.

Latra lazima iweke adhabu kali, ikiwemo kufuta leseni kwa wamiliki wa mabasi ambao wanaruhusu abiria kusafiri bila kusajiliwa ipasavyo kwenye mfumo. Sheria ya kuwa na manifesto tatu (kituoni, polisi na garini) lazima isimamiwe bila muhali.

Ili kufanikisha yote hayo, Serikali lazima iwekeze nguvu kubwa katika kutoa elimu kwa umma. Wananchi wanapaswa kuelewa kuwa kukata tiketi kwa njia ya kielektroniki ni ulinzi wao wa kwanza dhidi ya kuibiwa na walanguzi.

Aidha, kampuni za mawasiliano zishirikiane na Latra kuhakikisha kuna utengamo wa mtandao ili kusiwe na kisingizio cha "mtandao unasumbua" wakati wa kukata tiketi.

Hii ni muhimu kwa kuwa hatua ya kuelekea digitali katika usafirishaji si ya hiari, ni hitaji la lazima kwa maendeleo ya nchi.

Ndiyo sababu tunaitaka Latra isiishie kutoa matamko ya ukaguzi barabarani pekee, bali iweke mfumo dhabiti utakaofunga mianya yote ya fedha taslimu na kumlinda abiria.

Vilevile, Latra ihakikishe mfumo wa karatasi haupewi nafasi kurudi kwa kuwa kufanya hivyo ni sawa na kurudi gizani; hivyo ni lazima ishikilie mwanga wa teknolojia kwa usimamizi thabiti na kuchukua hatua badala ya kulalamika.

## KING KINYA




**HUTOLEWA NA MWANANCHI COMMUNICATIONS LIMITED (MCL)**


MWANANCHI COMMUNICATIONS LTD

Barabara ya Mandela, SLP 19754, Dar es Salaam
+255 22 24 50875, 0754 780647, 0765 864917
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Rosalynn Mndolwa-Mworia:** *Mkurugenzi Mtendaji*
**Mpoki Thompson:** *Mhariri Mtendaji Mkuu*
**Joseph Damas:** *Mhariri Mtendaji*
*Tunawezesha taifa*

CamScanner

USAFIRISHAJI



Kituo cha Mabasi cha Magufuli jijini Dar es Salaam. **Picha ya Maktaba**

# Sababu za mabasi kukacha stendi ya Magufuli zasakwa

**Bakari Kiango na Juma Issihaka,** Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Licha ya Serikali kutumia zaidi ya Sh50 bilioni kujenga Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli, bado mabasi hayo yanaendelea kushusha na kupakia abiria nje ya kituo na hivyo kukikosesha mapato.

Kufuatia hali hiyo, Serikali imeunda timu maalumu ya wataalamu itakayofanya tathmini ya kina ya uendeshaji wa stendi hiyo, itakayofanya kazi kwa siku 90.

Kituo hicho, kilichoanza rasmi kutoa huduma Februari 24, 2021, kilijengwa kwa lengo la kuboresha usafiri wa mabasi ya mikoani, kuondoa msongamano barabarani na kuweka utaratibu wa kisasa wa usafiri wa umma mikoani.

Hata hivyo, zaidi ya miaka minne tangu kifunguliwe, changamoto ya mabasi kutokitumia kituo hicho kushusha na kupakia abiria imeendelea kuwa mfupa uliokosa meno ya kuutafuna.

Ukiacha kukosa mapato yanayoenda kwenye Manispaa ya Ubungo, wajasiriamali na wakazi wa eneo hilo, wanasema hatua ya mabasi kupakia abiria nje ya kituo hicho, inaathiri biashara zao na malengo ya mradi.

### Ni mfupa mgumu

Mei 30, mwaka 2022, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Innocent Bashungwa, alitoa siku saba kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kukutana na wadau kuweka utaratibu wa mabasi kushusha na kupakia abiria ndani ya kituo.

Katika maelekezo hayo, alitaka mkuu huyo wa mkoa akutane na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra), Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (Taboa) na wadau wengine.

Katika ziara yake kituoni hapo, Bashungwa alisisitiza Serikali haitakubaliana na watu wasiofuata utaratibu uliowekwa, ikizingatiwa fedha nyingi zilitumika kujenga stendi hiyo.

Aidha, aliagiza kufanyiwa mapitio kiwango cha kodi ya pango kwa wapangaji wa stendi hiyo, kuondolewa kwa magari mabovu zaidi ya 40 yaliyokuwa yameegeshwa kwa muda mrefu na kuimarishwa kwa usimamizi wa shughuli za stendi hiyo.

Hivyo, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla alitangaza kuondoa katazo lililokuwa likizuia mabasi kupakia abiria au kushusha katika vituo binafsi na badala yake aliruhusu utaratibu huo kuendelea kwa sharti la kila basi kuingia ndani ya kituo cha Magufuli.

Uamuzi huo ulitolewa Agosti mwaka 2022 wakati wa kikao cha pamoja baina ya Latra, wamiliki wa stendi binafsi na Manispaa ya Ubungo na kubaini pasipokuwa na shaka kuwa, waliotengeneza vituo binafsi walifuata taratibu na kupatiwa vibali baada ya kukidhi vigezo.

**WASIFU WA STENDI**

**Stendi ya Magufuli, maarufu kama stendi ya Mbezi Louis, ni moja ya miundombinu mikubwa na ya kisasa ya usafiri wa mabasi nchini Tanzania. Ipo katika eneo la Mbezi, kando ya Barabara ya Morogoro jijini Dar es Salaam, na ilizinduliwa mwaka 2020 wakati wa uongozi wa Rais wa Awamu ya Tano, hayati John Pombe Magufuli, ambaye jina lake limepewa stendi hiyo.**

**Stendi hii imejengwa kwa lengo la kuboresha usafiri wa abiria, kupunguza msongamano wa mabasi katikati ya jiji na kuongeza usalama na ufanisi. Ina uwezo wa kuhudumia maelfu ya abiria kwa siku, ikiwa na mabasi yanayosafiri kwenda mikoa mbalimbali ya Tanzania na nchi jirani.**

**Miundombinu yake ni ya kisasa, ikijumuisha maegesho ya kutosha, ofisi za makampuni ya mabasi, huduma za usafi, mifumo ya usalama, maeneo ya biashara na huduma za kifedha.**

**Stendi ya Magufuli, licha ya changamoto zake, imekuwa kitovu muhimu cha usafiri na biashara, ikichangia ukuaji wa uchumi wa jiji na kuboresha uzoefu wa wasafiri.**

Miongoni mwa vigezo vilivyotolewa na Latra ili kuruhusiwa kuanzisha stendi binafsi ni kuwapo kwa vyoo, sehemu ya mapumziko kwa abiria, viburudisho na sehemu ya maegesho.

Kutokana na hilo, Makalla aliridhia vituo binafsi vitano vilivyohakikiwa kuendelea kutoa huduma na kufungua milango kwa wamiliki wengine wanaohitaji kuwa na vituo binafsi kushirikiana na Latra waanzishe.

Aidha, Makalla aliiagiza Manispaa ya Ubungo kukaa kikao mara moja na wamiliki wa stendi binafsi ili kuona njia bora ya ukusanyaji wa mapato.

Baada ya yote hayo, mwenendo wa mabasi kushusha na kupakia abiria nje ya stendi umeendelea kuwapo.

### Malalamiko mapya

Mjasiriamali katika kituo hicho, John Joseph, alisema mabasi mengi bado yanaegeshwa nje ya stendi badala ya kuingia ndani kama ilivyoelekezwa.

"Ni muda mrefu tangu tulipohamia hapa, lakini changamoto hii bado ipo. Mabasi mengi yanabaki nje badala ya kuingia stendi. Tunaomba Serikali itusaidie kulisimamia hili," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mshikamano, Herny Madenge alisema stendi hiyo ingeleta tija zaidi endapo mabasi yote yangelazimishwa kuitumia kikamilifu.

"Natamani sana mabasi yote yaishie hapa. Stendi ipo, miundombinu ipo, lakini matumizi yake bado ni hafifu," alisema.

> **"Changamoto zote mlizozitoa nimezipokea kwa niaba ya Waziri. Tuipe nafasi timu hii ifanye kazi ili tupate mwelekeo sahihi wa kwenda mbele kutoka hapa tulipo."**
>
> Reuben Kwagilwa

### Wamiliki mabasi wanena

Msemaji wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (Taboa), Mustapha Mwalongo alisema kumekuwa na ongezeko la mabasi yanayoihama stendi ya Magufuli na kuegesha pembezoni mwa hifadhi za barabara, kinyume cha utaratibu.

Ametaja maeneo ya Shekilango na Manzese kuwa miongoni mwa yanayotumiwa na baadhi ya mabasi kushusha na kupakia abiria bila kuingia stendi.

"Kuna mabasi yanayoanza safari na kupita Bagamoyo moja kwa moja bila kufika hapa stendi. Kwanza yanakwepa ushuru, pia kuna vibali vingi vinazidi kutolewa vya mabasi kuegeshwa nje ya stendi," alisema Mwalongo.

Alisema stendi hiyo ilijengwa kwa gharama kubwa, hivyo ni muhimu mabasi yote ambayo hayajakidhi vigezo vya kuwa na vituo binafsi yaingie ndani ya kituo hicho.

"Hili si suala la Taboa pekee, nimezungumza kama mdau wa stendi. Kama hali itaendelea hivi, stendi ya Magufuli itakufa kwa sababu hakuna gari litakaloingia hapa," alisema.

Hata hivyo, alisema yapo mabasi machache ambayo yamekidhi vigezo vya kuwa na vituo vyake binafsi, ikiwamo sehemu za kupumzika na huduma za chakula, lakini akadokeza mengi hayana sifa hizo.

"Wengine mtu ana ofisi moja tu, lakini anaegesha mabasi yake nje ya stendi. Hii si sawa," alisema.

### Uchunguzi kufanyika

Kutokana na malalamiko hayo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Reuben Kwagilwa, amemwagiza Katibu Mkuu, Adolf Ndunguru, kuunda timu maalumu ya wataalamu itakayofanya tathmini ya kina ya uendeshaji wa stendi hiyo.

Katika ziara yake kituoni hapo Desemba 23, 2025, Kwagilwa alisema timu hiyo itashirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na itajumuisha wataalamu wa sekta ya usafiri, watumiaji wa stendi na taasisi nyingine za Serikali zenye dhamana ya usafiri wa umma.

"Ifanyike tathmini ya mradi huu, ikihusisha malengo yake ya awali, ufanisi wake, miundombinu iliyopo, huduma zinazotolewa na mapato yanayopatikana na yanayopotea," alisema.

Alisema timu hiyo itapewa siku 90 kufanya kazi yake na kutoa mapendekezo yatakayosaidia Serikali kupata suluhisho la kudumu kuhusu matumizi sahihi ya stendi hiyo.

"Changamoto zote mlizozitoa nimezipokea kwa niaba ya Waziri. Tuipe nafasi timu hii ifanye kazi ili tupate mwelekeo sahihi wa kwenda mbele kutoka hapa tulipo," alisema.